

Swali hili liliandikwa na Yusuf Kalala wa Washington DC, akimuuliza Dr. Christopher Chacha Mwita (CCM), wa Alabama kuhusiana na Shairi lake aliloliandika katika lumbano la kishairi na Hassan Adam wa Cologne Ujerumani

WOSIA-SWALI

1. Leo tumepata siri, uwanjani imetokezea.
Ulingo wa mashairi, Chacha kauparamia.
Tena kavaa sihiri, shingoni imemuenea.
Jibu wamjibu nani, bora ukatuambia.
2. Hau "wosia (shairi), ndio alotuletea.
Akimkanya Bakari, mke kumwandalia.
Itamkuta khatari, mno aking'ang'ania.
Jibu wamjibu nani, mbona hukuelezea.
3. Huu "wosia wa Bakari," Kalala kazingatia.
Kuusifu uhodari, huku akishangilia.
Wa utungo mahiri, Hau katudhihirishia.
Jibu wamjibu nani, kati ya waliotokea.
4. Unalijibu "shairi, Hau alotuonyea.
Au "wosia wa Bakari," Kalala alopongezea.
Ujitokeze dhahiri, sio kwa kunyemelea.
Jibu wamjibu nani, mbona hukupambanua.

*Yusuf Kalala. (Washington, DC
Julai, 2002 SALAAM.*